# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## OFISI YA RAIS
## TUME YA UTUMISHI WA UMMA

Jengo la Chimwaga (UDOM), Ghorofa ya 2, 2 Barabara ya UDOM, S.L.P 1074, **40405 DODOMA.**
Nambari ya simu: 0738 166 703, 0733 005 974, Barua pepe: secretary@psc.go.tz, Tovuti: www.psc.go.tz

### TAARIFA KWA UMMA

### KUANZA MATUMIZI YA MFUMO WA KIELEKTRONIKI WA KUSHUGHULIKIA RUFAA NA MALALAMIKO WA TUME YA UTUMISHI WA UMMA

Kifungu cha 12(1)(d) na 27(1)(b) vya Sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298 [Marejeo ya Mwaka 2023] kinaipa Tume ya Utumishi wa Umma mamlaka ya kupokea na kushughulikia rufaa za Watumishi wa Umma. Aidha, Kanuni ya 73(1)(b) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za Mwaka 2022 inaipa Tume mamlaka ya kushughulikia malalamiko ya Watumishi wa Umma ambao hawakuridhishwa na uamuzi wa Waajiri, Mamlaka za Ajira na Mamlaka za Nidhamu katika usimamizi na uendeshaji wa Masuala ya Ajira na Nidhamu katika Utumishi wa Umma.

Tume ya Utumishi wa Umma imejenga Mfumo wa Kielektroniki wa Kushughulikia Rufaa na Malalamiko ya Watumishi wa Umma (PSCMIS). Mfumo huu utasaidia Watumishi wa Umma kuwasilisha kwa urahisi na kwa wakati rufaa na malalamiko yao Tume ili yaweze kushughulikiwa. Aidha, utasaidia Waajiri, Mamlaka za Ajira na Mamlaka za Nidhamu kuwasilisha Tume vielelezo vya rufaa na malalamiko ya Watumishi wa Umma na kupata mrejesho kwa wakati kuhusu rufaa na malalamiko hayo.

Mwezi Februari 2025, Tume iliutambulisha Mfumo huu kwa Wadau wake na kutoa mafunzo kuhusu namna utakavyotumika. Hivyo, napenda kutoa taarifa kwa Wadau wote na umma kwa ujumla kuwa Mfumo huu sasa upo tayari na utaanza kutumika tarehe **15 Januari, 2026.**

Mfumo huu unapatikana kwa anwani ya ***portal.psc.go.tz***. Kwa taarifa zaidi tafadhali wasiliana na **Bw. Justine Jackson** kwa namba ya Simu **0786 479 345** na **Bw. Markson Senguji** kwa namba ya Simu **0747 298 068.**

John C. Mbisso
**KAIMU KATIBU**
**TUME YA UTUMISHI WA UMMA**